



## EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

### **MAOMBI YA KUONYESHA NIA YA KUKODISHA NAFASI/OFISI YA BIASHARA KWA AJILI YA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP) KUMBUKUMBU NA. 0010006583**

Kampuni ya TOTAL East Africa Midstream B.V Tanzania, kampuni ya Mafuta na Gesi, inaalka makampuni yenye uzoefu na sifa kutuma nia ya kukodisha nafasi/ofisi kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa ardhini na litakalovuka mipaka ya nchi la kusafirisha Mafuta ghafi kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni karibia kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

#### **MAELEZO MAFUPI YA UWANDA WA HUDUMA:**

Mradi unahitaji eneo kwa ajili ya matumizi ya ofisi kwa ajili ya timu yake ya kibiashara na timu ya Mradi inayokua. Timu zinatarajiwa kukua kwa haraka mwanzoni mwa robo ya tatu (Q3) ya mwaka 2021 na kukaribia takribani watu 300 ndani ya mwaka ujao. Nafasi yenye ukubwa wa mita za mraba 1000 itahitajika hadi kufikia robo ya tatu (Q3) ya mwaka 2021 na uhitaji kuongezeka hadi kufikia ukubwa wa mita za mraba 3,500 mpaka 3,700 katika kipindi cha miaka miwili.

Pendekezo la eneo ni Masaki au karibu na eneo la Masaki na/au maeneo ya Oyster Bay likiwa na miundombinu ya kutosha kwa ajili ya kuhifadhi magari. Masuala ya usalama wa wafanyakazi na ulinzi ikiwemo vyombo vinavyojitoshesha vya kujikinga dhidi ya moto na moshi, njia maalumu ya kujiokoa na eneo maalum la kukusanyika nyakati za Dharura, eneo la kuingilia linalolindwa na lenye sehemu ya walinzi, jiko pamoja na vifaa vya usafi. Mseto wa ofisi binafsi, za pamoja, pamoja na maeneo huru ya kufanyia kazi kwa pamoja yatatiliwa maanani. Vyumba vya ukubwa tofauti tofauti kwa ajili ya matumizi ya kuendesha vikao vinahitajika.

#### **VIGezo MUHIMU:**

Makampuni yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa usajili chini ya Sheria za Tanzania.
- Uthibitisho wa leseni ya biashara.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) (Vyeti vya Nambari ya Mlipa Kodi na Usajili wa Kodi ya Ongezeko la Thamani) na Cheti cha Ithibati ya Malipo ya Kodi cha mwaka wa hivi karibuni.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: [talal.mufti@external.total.com](mailto:talal.mufti@external.total.com) (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa 11:00 jioni Majira ya Afrika Mashariki, Jumatatu tarehe **2 Machi 2021**.

**Muhimu: Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapatia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).**